

ASILI YA BIASHARA YA MALIPO YA KIDOGOKIDOGO NI HALALI



“ Mfano kuna mtu alikuwa anahitaji bajaji lakini hana pesa ya kutosha kununua bajaji akaenda kwenye kampuni zinazouza bajaji na wanatoa kwa mkopo pia. Miongoni mwa vigezo **lazima awe na pesa ya kianzio ambayo waliweka ni milioni 1 au milioni 2**, ukishatoa hiyo wanakupa bajaji ukafanye kazi lakini utalipa kidogokidogo kwa muda wa mwaka **mmoja** au wewe utakavyosema waweza waaambia nitalipa kwa mwaka au mwaka na nusu au isizidi miaka miwili. Lakini jumla ya pesa utakayolipa kwa huo muda uliouchagua mwenyewe inakuwa ni kiasi cha shilingi milioni 11 na laki moja. Je muamala kama huu umekaaje? Baarakallaahu fiyk ”

Hilo ni swali la ndugu yetu ambaye amesoma makala zetu tulizozituma katika grupu letu la MARKAZ IBNU UTHAIMIN DODOMA kuhusu miamala ya riba. Tunamuomba asome maswali mawili yafuatayo yenyewe kufanana na hilo kisha asome majibu ya wanachuoni kama ifuatavyo;

س شخص يقول أنا رجل أملك مبلغاً من المال واستثمره في شراء سيارات نقداً، ثُم السيارة تسعه آلاف ريال أبيع السيارة بالتقسيط لمدة سنة وستين بملبغ أربعة عشر ألفاً أو عشرة آلاف ريال بعد أن آخذ مقدماً ألفي ريال أو ثلاثة آلاف ريال وأنا في شكل هل هذا البيع صحيح أو ربا وما حكم ما سبق في هذا البيع علمأً أن لي مدة ستين بهذه الطريقة؟.

ج لقد أحل الله البيع وحرم الربا فقال تعالى (وأحل الله البيع وحرم الربا) وكان مما أحله من البيع، البيع إلى أجل، يدل على مشروعية ذلك قوله تعالى (يأيها الذين آمنوا إذا تدابنتم بدين إلى أجل مسمى فاكتبوه وليكتب بينكم كاتب بالعدل ولا يأب كاتب أن يكتب كما علمه الله) الآية. قال القرطبي في تفسيره ((هي تتناول جميع المدابنات إجماعاً)) ، ثبتت في الصحيحين عن عائشة رضي الله عنها أنها أهلتها بتسع أواق تسعة أقساط، في كل عام أوقية، فأقر ذلك النبي ﷺ وهذا يعلم جواز التعامل بالصورة التي سأل عنها السائل لدخولها في عموم الآية. وبالله التوفيق وصلى الله على نبينا محمد وآله وصحبه وسلم.

SWALI

Mimi ni mtu ninayemiliki kiasi fulani cha pesa na ninakizalisha kwa kununua magari kwa cash (malipo ya pamoja) kwa bei ya Riali elfu 9. **Ninauza gari hizo kwa malipo ya kidogokidogo kwa muda wa mwaka mmoja au miaka miwili kwa kiwango cha Riali elfu 14 au elfu 10**, baada ya kuwa nimechukua (kutoka kwa mmunuzi) **malipo ya utangulizi Riali elfu 2 au elfu 3**. Nami nina wasiwasi Je, biashara hii ni sahihi au ni riba, na ipi hukumu ya biashara yangu kwa njia kama hii ambayo nimekuwa nayo tangu miaka miwili iliyopita ?

JAWABU:

Hاكika Allah amehalalisha biashara na ameharamisha riba, amesema Allah Mtukufu ((Na Allah amehalalisha biashara na ameharamisha riba)); **na miongoni mwa biashara aliyoihalalisha ni biashara ya malipo ya (kidogokidogo kwa) muda maalumu**. Kauli ya Allah ifuatayo inajulisha juu ya usheria wa hilo; ((Enyi mlionaini pindi **mtakapouza au kununua kwa deni mpaka muda maalumu**, basi andikianeni....)) Amesema Imam Alqurtubiy Allah amrehemu; (kuhusu maana ya aya hiyo); “Aya hiyo inakusanya madeni yote, kwa makubaliano ya wanachuoni”

Na imethibitika ndani ya Bukhari na Muslim masimulizi kutoka kwa Aisha Allah amridhie amesema ; hakika (mtumwa wa kike ait-waye) Barirah **aliuzwa** na wasimamizi wake kwa kiwango cha Waqia 9 **kwa malipo ya kidogokidogo kwa muda wa miaka tisa**, Mtume ﷺ akalikubali hilo (wala hakulikemea) , hii inajulisha kufaa kufanya muamala kwa sura hiyo ambayo ameiulizia muulizaji, kwa sababu inaingia katika (uhalali wa) ujumla uliopo katika aya.'

س ذهبت إلى إحدى الشركات التي تبيع سيارات بالتقسيط واشترت منها سيارة أفادوني أنها نقداً بـ 50500 ريال وتقسيطاً بـ 54131 أي بزيادة 14 على المتبقى من المبلغ دفعت لهم 10000 والباقي 44131 مقططة على 12 شهراً، استلمت السيارة وبعد مضي 4 شهور فكرت مصادفة في المبلغ الزائد، ذهبتأسأthem ما هي الـ 14 أفادوني أنها مصاريف بنكية فبدأ الشك لدى فهل ما تم حرام أم حلال؟
ج إذا اتفق المشتري لأجل مع شركة السيارات بأن المبلغ 54131 كله ثمن للسيارة يدفع أقساطاً أو يدفع بعضه عاجلاً وبعضه آجالاً فالبيع جائز شرعاً ولو كان الثمن المؤجل أكثر من الثمن نقداً

SWALI

Nilikwenda katika kampuni moja ambayo inauza magari kwa **malipo ya kidogokidogo** na nikanunua gari wakanieleza kwamba gari linauzwa Riali elfu 50 na mia tano kwa malipo ya pamoja, **na linauzwa kwa Riali elfu 54 na mia moja na thelathini na moja kwa malipo ya kidogokidogo** yaani ongezeko la asilimia 14. **Nikawatangulizia malipo ya Riali elfu 10**, na pesa iliyobaki yaani Riali elfu 44 na mia moja na thelathini na moja **nikailipa kidogokidogo kwa muda wa miezi 12** ; **ki-sha nikakabidhiwa gari**, na baada ya kupita miezi 4 ghafla nikaanza

kufikiria kiwango kilichozidi nikaenda kuwa uliza kuhusu asilimia 14 iliyozidi wakaniambia kuwa ni gharama za kibenki. Hapo nikaanza kupa wa siwas kuhusu muamala uliofanyika ni wa haramu au wa halali....?

JAWABU

Pindi mnunuzi anapokubaliana na kampuni (kununua gari) kwa malipo ya kidogokidogo **kwa muda maalumu**, kwa kiwango cha Riali elfu 54 na mia moja na thelathini na moja ambayo ni bei ya gari atakayoilipa yote kidogokidogo, **au baadhi atailipa kwa kuitanguliza kisha iliyobaki atailipa kidogokidogo**, biashara hiyo **infaa kisheria** hata kama bei ya ulipaji wa kuchelewesa (kidogokidogo) ni kubwa zaidi kuliko bei ya malipo ya pamoja.'

Hitimisho:

Kulingana na majibu ya wanachuoni,tunafahamu kuwa biashara ya namna hiyo infaa kisheria maadamu masharti yawe yamechungwa. Mionganoni mwa masharti hayo ni; **Muuza ji awe anauza bidhaa ambayo anaimiliki**, **Wakubaliane kiwango cha malipo** , **Wakubaliane kiwango maalumu cha muda wa malipo hayo**, **Malipo yasiongezeke kwa sababu ya kuchelewa kulipa ndani ya wakati waliokubaliana** n.k Tutaona uchambuzi wa masharti hayo katika makala zijazo inshaa Allah. Endelea kuwa nasi , Allah atubariki kwa chumo la halali.

وصلى الله على محمد وعلى آله وصحبه وسلم

Mkusanyaji na Mkalmani: Ummati Abdallah, Abuu Muhammad

المصدر : اللجنة الدائمة للبحوث العلمية والإفتاء